

## **Programu ya WIC ya Iowa-Makubaliano ya Mteja Haki na Wajibu wa Mshiriki**

### **Naelewa kwamba:**

- Nitapokea misaada ya WIC ili niweze kununua vyakula vinavyokidhi viwango. Naelewa kwamba misaada ya WIC haina vyakula vyote na maziwa yote ya fomula kwa mwezi mmoja ukizingatia kwamba ni mpango wa nyongeza.
- WIC itanipatia vionjo kuhusu namna ya kuitunza familia yangu kwa vyakula vyenye afya.
- WIC itanisaidia kupata Daktari na itanipa rufaa kuhusu vitu kama chanjo kwa ajili ya watoto wangu. WIC inaweza kunipa taarifa kuhusu afya au huduma za kijamii ninazozihitaji.
- Nina haki ya kusikilizwa vizuri iwapo sijakubaliana na na maamuzi yatakayokuwa yamechukuliwa kuhusu kukubaliwa kwangu kupewa misaada ya WIC. Naelewa kwamba natakiwa kuandika barua au kupigia simu Ofisi yangu ya WIC ndani ya siku 60 baada ya kupokea barua ya maamuzi, ili niweze kupata kusikilizwa vizuri.
- Watumishi wa WIC watanipa heshima stahiki. Viwango vya kuchaguliwa na kushiriki kwenye Programu ya WIC ni sawa kwa kila mmoja. Iwapo nitahisi kwamba nimebaguliwa kwa misingi ya kikabila, rangi, asili ya uraia, jinsia, umri au ulemavu, naweza kufungua mashtaka kwenye anuani iliyopo kwenye boksi hapo chini.
- Shirika la karibu litafanya huduma za afya, elimu ya chakula na msaada wa unyonyeshaji unaoweza kupatikana na nasisitizwa kushiriki kwenye huduma hizi.

### **Mshiriki wa WIC:**

- Nitanutua tu vyakula vilivyoainishwa kwenye orodha ya misaada yangu ya WIC. Nitatumia vyakula vya WIC tu kwa ajili ya Programu. Iwapo nitashiriki uhifadhi wa motto/watoto wangu, nitahakikisha kwamba chakula cha WIC kinachangiwa na watoto wangu.
- Nitatumia misaada ya WIC na/au kadi ya WIC niliyopewa tu. Sitafanya biashara, kuuza, kubadilisha au kusafirisha, au kujaribu kufanyia biashara, kuuza, kusafirisha au kubadilisha, chakula/maziwa au misaada niliyopewa. Sitaruhusu mtu yeyote mwingine kufanyia biashara, kuuza, kusafirisha au kubadilisha, au kujaribu kufanyia biashara, kuuza, kusafirisha au kubadilisha chakula chochote au maziwa ya formula au misaada niliyopewa.
- Nitatunza stakabadhi zote za mauzo kwa muda wa miezi mitatu ya chakula/maziwa kilichotolewa na WIC na ambacho hakikunuliwa kwa kutumia Kadi yangu. Stakabadhi zitafanya kazi kama ya ushahidi nitakaotoa kwenye Programu ya WIC, ikihitajika, kuthibitisha kwamba sihusiki moja kwa moja au kwa mbali na yafuatayo:
  - Kufanyia biashara, kuuza, au kuhamisha au kubadilishana chakula chochote au formula iliyotolewa na Mpango wa WIC kwa ajili ya fedha, mikopo, vitu ambavyo siyo chakula, au vyakula ambavyo havijaidhinishwa ikiwa ni pamoja na chakula (zaidi) ya kilichoidhinishwa na / au
  - Kujaribu kufanyia biashara, kuuza, au kuhamisha au kubadilishana kila aina ya chakula au formula iliyotolewa na mpango wa WIC kwa ajili ya fedha taslimu, mikopo, bidhaa zisizo za chakula, au vyakula visivyoidhinishwa ikiwa ni pamoja na chakula zaidi ya kilichodhinishwa. Jaribio linajumuisha kutoa ofa kwa mdomo moja kwa moja au kwa mbali, kwa kuchapishwa, au mtandaoni kupitia tovuti kama vile Craigslist, Facebook, eBay, au tovuti nyinginezo.
- Ninaelewa kwamba sitapata fidia ya misaada ikiwa zitapotea au kuibiwa.
- Ninaelewa kuwa vifaa vyote vya WIC nilivyoazimwa au nilivyokopeshwa vitatumiwa tu kwa kusudio lake. Pia ninaelewa kuwa kama vifaa vilipotea, vimeharibiwa, vimeibiwa au havirudishwi kwa wakati kwa wakala wa ndani, nitawajibika kwa gharama ya kununua vingine.

- Uaminifu wa kawaida: Nitawafanyia wafanyakazi wa WIC, watumishi wa maduka au wateja, na mali kwa heshima na kwa uaminifu. Ninaelewa kuwa mimi, au mmoja wa washirika wangu, anaweza kupoteza misaada yangu ya chakula cha WIC kwa kusema kwa kudhalilishisha, kumsumbua, kutishia au kuumiza kimwili mfanyakazi wa WIC, mteja au mtumishi wa dukani.
- Nitafika kwenye apointmenti zangu au nitapiga simu kabla ikiwa siwezi kufika. Ikiwa sina misaada ya chakula iliyotolewa kwa miezi mitatu mfululizo, nitasimamishwa kutoka kwenye programu.
- Nitapata misaada ya chakula cha WIC kutoka kliniki moja tu kwa wakati mmoja. Ushiriki wa mara mbili ni kinyume cha sheria.
- Ninaelewa kwamba ikiwa nihamia eneo jipya la huduma ya WIC, ninastahili kuomba na kupokea fomu ya uthibitisho ambayo inaniruhusu kuhamisha WIC yangu kwenye eneo langu mpya kwa muda uliyothibitishwa. Ninaelewa ni lazima nitoe vyombo vyovyote vya chakula visivyotumiwa au kadi kutoka jimbo nilikotoka kwenye ofisi yangu mpya ya WIC kabla ya kunipa misaada katika jimbo lao.
- Nitajulisha wakala wa WIC wa eneo langu mabadiliko yoyote makubwa ambayo yanaweza kutokea kama taarifa zangu za mawasiliano, mabadiliko ya jina, na mabadiliko ya uhifadhi kwa watoto walio chini ya uangalizi wangu ambao wanapokea huduma za WIC.
- Nitaruhusu uchunguzi wa afya wa WIC kwa waombaji wote wa WIC katika familia yangu. Ufuatiliaji wa afya wa WIC ni pamoja na kujibu maswali ya afya na mlo, kupima urefu, uzito, na kupima kiwango cha madini ya chuma kwenye damu.
- Ninaelewa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Afya ya Umma ya Iowa anaweza kuidhinisha uchangiaji wa taarifa zangu za WIC na asasi maalumu za kiafya na kielimu. Asasi hizi zinaweza kutumia taarifa hizi kuamua iwapo nastahili kushiriki kwenye programu zao; kunipatia taarifa juu ya programu hizo na kufanya mchakato wa maombi kuwa rahisi; kuboresha afya yangu, elimu au ustawi ikiwa nimejiunga na mipango yao; na kuhakikisha mahitaji yangu ya huduma ya afya yamepatiwa ufumbuzi. Taarifa hii itatumiwa na mashirika ya WIC na mashirika ya umma katika usimamizi wa mipango yao ambayo hutumiwa kwa watu waliyochaguliwa kwenye Mpango wa WIC. **Ninaelewa kwamba IDPH inaweza pia kuidhinisha ugawaji wa habari yangu ya WIC kama inavyotakiwa au imeidhinishwa na sheria za serekali.** Ninaweza kuomba orodha ya programu za IDPH ambazo zitapewa taarifa yangu ya WIC kama ilivyoainishwa katika Sera ya WIC 245.05.
- Nimeshuriwa kuhusu haki na majukumu yangu chini ya Mpango. Ninathibitisha kwamba taarifa niliyoiweka kama kigezo cha kuchaguliwa kwangu ni sahihi, kwa ukweli wangu wote. Fomu hii ya uthibitisho imewasilishwa kuhusiana na kupokea msaada wa Shirikisho. Maofisa wa Programu wanaweza kuthibitisha habari kwenye fomu hii. Ninaelewa kwamba kwa makusudi kutoa taarifa ya uwongo au ya kupotosha, kwa kuficha, au kuficha ukweli kunaweza kusababisha kulipa shirika la serikali, kwa fedha taslimu, thamani ya misaada ya chakula niliyopewa kinyume cha utaratibu na naweza kushtakiwa chini ya mjibu wa sheria za kiraia au za jinai za Serikali ya Shirikisho.
- Ninaelewa kwamba kukiuka sheria ya Shirikisho, sheria ya serikali, au hati hii inaweza kumaanisha kusitishwa kwa Mpango wa WIC kwangu.

Jina la mshiriki wa WIC anayethibitishwa leo:

---



---

Saini ya mshiriki / mzazi / mlezi

Tarehe

Kwa mujibu wa Sheria ya Haki za kiraia na Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA) ya sera za kiraia, USDA, Wakala zake, ofisi, na wafanyakazi, na taasisi zinazohusika au kuendesha mipango ya USDA zinakatazwa kufanya ubaguzi kwa misingi ya rangi, asili ya uraia, jinsia, ulemavu, umri, au kulipiza kisasi kwa shughuli za haki za kiraia kabla ya mpango wowote au shughuli iliyofanywa au kufadhiliwa na USDA.

Watu wenye ulemavu wanaohitaji njia mbadala za mawasiliano kwa taarifa ya programu (k.m. Braille, machapisho makubwa, mikanda ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani, nk), wanapaswa kuwasiliana na Shirika la (la kiserikali au kieneo) ambapo waliomba misaada. Watu ambao ni viziwi, wenye matatizo ya kusikia au wenye matatizo ya kuzungumza wanaweza kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Usambazaji wa Shirikisho kwenye namba (800) 877-8339. Zaidi ya hayo, maelezo ya programu yanaweza kupatikana katika lugha nyingine tofauti na Kiingereza.

Ukitaka kutoa malalamiko ya ubaguzi, kamilisha Fomu ya Programu ya Malalamiko ya Ubaguzi, (AD-3027) inayopatikana mtandaoni: [http://www.ascr.usda.gov/complaint\\_filing\\_cust.html](http://www.ascr.usda.gov/complaint_filing_cust.html), na kwenye ofisi yoyote ya USDA, au uandike barua itakayopelekwa kwa USDA na kutoa taarifa iliyoombwa kwenye fomu katika barua. Kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, simu (866) 632-9992. Tuma fomu yako kamili au barua kwa USDA kwa:

(1) Barua: U.S. Department of Agriculture  
Office of the Assistant Secretary for Civil Rights  
1400 Independence Avenue, SW  
Washington, D.C. 20250-9410;

(2) Faksi: (202) 690-7442; or

(3) Barua Pepe: [program.intake@usda.gov](mailto:program.intake@usda.gov).

Taasisi hii ni mtoa fursa sawa.